# MISINGI YA IMANI #1

Mpendwa mwanafunzi,

Hongera kwa kumaliza Sehemu ya Utangulizi wa Masomo. Hivi sasa ukuaji wako wa kiroho na wa mwenendo wako wa kikristo vitaimarishwa kulingana na utayari wako wa kujifunza Neno la Mungu. Ninaamini utabarikiwa mno kwa kuendelea kujifunza.

Pamoja na barua hii utakuwa umepewa somo la kwanza la "Misingi ya Imani" kwa ajili ya kuendelea kujifunza Biblia. Somo hili lina masomo mawili. Yameandaliwa kwa undani kidogo kuliko kozi ya utangulizi na masomo yote mawili yatakusaidia kujifunza kikamilifu zaidi habari za Biblia.

Kwa sasa unapaswa kujisikia vizuri unapofungua kurasa za Biblia. Mwanzoni ili Kuielewa Biblia, unaweza kuikuta mistari ya vifungu imefupishwa. Mfano: 1 The 2:7b inasimama badala ya Wathesalonike wa kwanza sura ya pili, mstari wa saba; lakini "b" ya mwishoni inaashiria nusu ya mstari. Vifupi vingine ni rahisi kuliko vingine. Fanya kila uwezalo kuielewa habari, lakini ukikutana na ugumu, usiogope kuomba msaada kwa Wakristo wengine.

Endelea na kazi nzuri na Mungu akubariki sana kadiri unavyodumu kuwa mwaminifu kwake!

Katika yeye,

Viongozi wa Masomo

## SEHEMU YA KWANZA

Somo hili linaendea kutilia mkazo msingi wa kweli wa injili isiyo ya kidhehebu. Limeandaliwa kuwaelekeza wanafunzi juu ya mpango wa Mungu kuhusu maisha yao na kuhimiza ushirika wao katika Yesu Kristo.

ZINGATIA: Mwanzoni mwa kila swali utakuta "anuani ya Maandiko." Anuani hii ni sura na mstari wa Biblia na utakusaidia kujibu swali. Kwa mfano: Yohana 3:16 inamaana Injili ya Mtakatifu Yohana, sura ya 3 na mstari wa 16. Tafuta jibu sahihi kutoka katika mstari na ulijaze katika nafasi iliyowazi kwa mwandiko mzuri. Unaweza kukijua kifungu kingine kinachotoa jibu la swali hili; lakini kwa somo hili, mwanafunzi anaombwa kukifuata kifungu alichopewa tu. Kama una maswali yoyote kuhusu somo hili, jisikie huru kuyaandika na kuyauliza.

Angalia jinsi ya kuwa Mberoya Muungwana (Matendo 17:10,11). *"Walilisikia* (Waberoya) *Neno kwa uelekevu wa moyo na kuchunguza Maandiko kila siku, waone kwamba mambo* (Mtume Paulo) *aliyoyasema yalikuwa kweli."*

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, Mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la Kweli."* (2 Timotheo 2:15)

*"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki."* (2 Timotheo 3:16)

ZINGATIA: Hakikisha unaomba, umwombe Mungu ayafungue macho yako ya ufahamu. Mtume Paulo aliwaombea waumini wa Kolosai na Efeso. Tunaweza kuyafanya maombi haya kuwa ya kwetu (Waefeso 1:16-18; na Wakolosai 1:9,10).

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

# KUANZIA KICHWANI HADI KIDOLENI MWANADAMU NI MWENYE DHAMBI HII NDIO MAANA YA NENO "UPOTOVU AU MKENGEUKO HALISI"

## SEHEMU IFUATAYO INAHUSU WARUMI 3:9-24

1. (Warumi 3:10,11) Wangapi ni wenye haki? _____

   Wangapi wanamtafuta Mungu? _____

2. (Warumi 3:13-15) Mtu asiye mwenye haki ana sifa gani?

   Koo _____

   Ndimi _____

   Midomo _____

   Vinywa _____

   Miguu _____

3. (Warumi 3:9-11) Kuna kitu chochote kuhusu mtu asiye haki ambacho Mungu anapendezwa nacho? _____

4. Nafasi ya mwanadamu katika asili yake mbele ya Mungu ni nini? (Warumi 3:23) _____

   _____

5. Mtu asiye haki atawezaje kuhesabiwa haki? (Warumi 3:24) _____

   _____

## SEHEMU IFUATAYO INAHUSU WAEFESO 2:1-3

6. (Waefeso 2:1) Watu wamekufa kiroho kutokana na nini? _____

7. (Waefeso 2:2; 4:27; 6:11; 2 Wakorintho 4:4) "Mfalme wa uwezo wa anga" ni nani? _____

8. (Waefeso 2:3) Kabla ya "kuhuishwa" au "kufanywa hai" katika Kristo wanadamu walikuwa nini katika asili yao? _____

**SIMAMA HAPA!**

Tutaendelea na somo letu baadaye kidogo, lakini kwanza chukua muda kidogo kutafakari sehemu hii ya Neno la Mungu ambalo umeshajifunza. Inasema nini kuhusu kila mmoja wetu? Tunakuomba ufanye hivyo kwa sababu ni muhimu kwa kila mtu kuuangalia hitaji lake la kuwa na Mwokozi. Je, Umeona hali ya kupotea kwako? Umeliona hitaji lako la kumpokea Kristo kama Mwokozi wa maisha yako? Tunaomba jibu lako liwe NDIYO!

Soma Injili (habari njema) katika1 Wakorintho 15:1-6, halafu soma Waefeso 1:7 na 2 Wakorintho 5:17. Yesu Kristo alikufa msalabani kulipia gharama ya dhambi zetu. Kwa imani katika Yeye, damu yake itakusafisha toka dhambini na kukufanya uwe kiumbe kipya katika Kristo.

## KATIKA SEHEMU HII TUTAANGALIA WARUMI 6:23.

9. A. Mshahara wa dhambi ni nini? _____

   B. Karama ya Mungu ni nini? _____

Kifo, maana yake ni kutengana na Mungu kwenda Jehenamu. Uzima wa milele, maana yake ni kuwepo na Mungu Mbinguni

10. Zawadi ya bure ya Mungu huja kumpitia nani? _____

11. Je umeipokea zawadi hiyo? _____

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

**KATIKA SEHEMU HII TUTAANGALIA 2 WATHESOLANIKE 1:7-11.**

12. (2 Wathesolanike 1:8) Kisasi cha Kristo kitakuja juu ya nani? _____

    _____

13. (2 Wathesolanike 1:9) Wataadhibiwa kwa muda gani? _____

14. Katika mstari wa 9 tunasoma jinsi waovu watakavyohukumiwa, wakati huohuo, katika mstari wa 10, tunasoma jinsi watakatifu (waumini) watakavyobarikiwa. Ni ombi gani Paulo alilowaombea waumini katika 2 Wathesolanike 1:11-12? _____

    _____

**KATIKA SEHEMU HII TUTAANGALIA WARUMI 5:1-8.**

15. (Warumi 5:1) Tunapata nini tunapohesabiwa haki kwa imani? _____
16. (Warumi 5:2) Tunafurahi katika nini? _____
17. (Warumi 5:3) Kama waumini tunapaswa kufanya nini wakati wa dhiki au mateso? _____
18. (Warumi 5:3) Mungu hutumia nini kuleta uvumilivu au saburi? _____
19. (Warumi 5:6,8) Tulikuwa na hali gani wakati Yesu alipotufia? _____

    _____

Shetani anafurahia kutuweka katika hali ya wasiwasi kuhusu wokovu wetu. Lakini Mungu, kupitia Neno lake, anatupa uhakika halisi kuhusu wokovu wetu na uzima wa milele tulio nao.

*"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu."* (1 Yohana 5:13)

20. (1 Yohana 5:13)

    A. Yohana aliwaandikia nani? _____

    B. Alikuwa na lengo gani? _____

21. (1 Yohana 5:11,12)

    A. Nani hutupa uzima wa milele? _____

    B. Uzima wa milele unapatikana katika nani? _____

    C. Nani wanao uzima wa milele? _____

    D. Nani hawana uzima wa milele? _____

22. Kulingana na Warumi 8:38-39, ni kitu gani kinachoweza kututenga na upendo wa Kristo? Zungushia jibu sahihi:

    (1) Kifo (2) Hatari (3) Nguvu za giza (4) Hakuna

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

# SEHEMU YA PILI

a. Warumi 3:9-24 inaeleza kwamba mwanadamu hana haki kabisa; sheria imeleta hukumu juu ya mtu muovu; na wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.
b. Waefeso 2:1-3 na Waefeso 5:6 inaeleza zaidi kuwa mwanadamu katika asili yake ni mtoto wa hasira (hasira ya Mungu) na amekufa kiroho. Yesu Kristo tu anaweza kumfanya mtu kuwa hai kiroho.
c. Warumi 6:23 inatueleza kuwa mshahara wa dhambi ni mauti na zawadi ya Mungu ni uzima wa milele kumpitia Yesu Kristo.
d. 2 Wathesolanike 1:7-12 inabainisha kuwa wanadamu wanaweza kuwekwa katika makundi mawili: wale wanaokusudiwa kwa hasira ya Mungu na wale wanaokusudiwa kwa utukufu wa Mungu.
e. Warumi 5:1-8 inaeleza jinsi Mungu alivyothibitisha upendo wake kwetu wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi, yaani wakati huo Kristo alikufa kwa ajili yetu. Pia inaeleza tuna amani na Mungu kwa imani katika Kristo.
f. Warumi 8:35-39 inatueleza kuwa hakuna kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Yesu Kristo Bwana wetu.

1. (2 Timotheo 3:16a) Maandiko yalitolewaje kwetu? _____
2. (2 Petro 1:21b) Nini maana ya “Biblia ni yenye pumzi ya Mungu”? _____

   _____
3. (1 Wakorintho 2:14) Mtu wa tabia ya asili asiye na Roho Mtakatifu hawezi kuyaelewa mambo ya Mungu. Kwa nini hawezi? _____
4. Warumi 8:9 inamwelezaje mtu wa kiroho? _____

   _____

   Mstari huu unamwelezaje mtu wa asili? _____
5. Kulingana na Yohana 3:3, lazima kifanyike nini ili mtu wa asili awe mtu wa kiroho?_____
6. Kunatokea nini wakati mtu wa asili anafanyika kuwa mtu wa kiroho kulingana na 2 Wakorintho 5:17? _____

   _____
7. Ili tubadilishwe kutoka mtu wa asili kuwa mtu wa kiroho, Yohana 20:31 inasema tufanye nini? _____

   _____
8. Warumi 10:9 inasema tufanye nini ili tuokoke? _____

   _____
9. Yohana 1:12a inasema lazima tufanye nini ili tuwe “watoto wa Mungu”? _____

   _____
10. (Warumi 8:9) Wewe ni nani, mtu wa kiroho au mtu wa asili? _____

**SOMA INJILI, “HABARI NJEMA” - 1 WAKORINTHO 15:1-6**

11. (2 Wakorintho 4:3) Injili imefichwa kwa akina nani? _____
12. Nani amewapofusha wasioamini? (2 Wakorintho 4:4) _____
13. Soma 1 Wakorintho 15:21-22 na Warumi 5:12. _____ (Weka vema kama umesoma)

    Nani aliileta dhambi na mauti ulimwenguni? _____

    Kwa nini kifo kimerithiwa na watu wote? _____

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

14. (Warumi 5:8) Mungu alioneshaje upendo wake kwetu tulipokuwa tungali wenye dhambi? _____

    _____

15. (Waefeso 1:17,18) Mungu anawezaje kuyafumbua macho ya ufahamu wako? _____

    _____

16. (Yakobo 1:5) Tunawezaje kupokea hekima na ufahamu kutoka kwa Mungu? _____

17. Kulingana Tito 3:5, tunaweza kufanya kazi yoyote ili tustahili kuokolewa? _____

    Kwa nini alituokoa? _____

    Alitumia njia gani kutuokoa? _____

18. Soma Waefeso 2:8,9; 1 Wakorintho 15:1-6; Warumi 1:16, halafu fikiria tena maswali uliyojibu hapo juu kabla hujajibu KWELI au HAPANA kwa maswali yafuatayo (weka vema katika nafasi husika):

    a. Ili aokoke ni lazima mtu kwanza ajiunge na kanisa. Kweli _____ Hapana _____
    b. Ili aokoke ni lazima mtu kwanza abatizwe kwa maji. Kweli _____ Hapana _____
    c. Ili aokoke ni lazima mtu aahidi kuishi maisha mazuri, safi na ya uadilifu. Kweli _____ Hapana _____
    d. Ili aokoke ni lazima mtu aifuate sheria ya Musa. Kweli _____ Hapana _____
    e. Ili aokoke ni lazima mtu aishi kwa utawala wa hali ya juu. Kweli _____ Hapana _____
    f. Ili aokoke ni lazima mtu aamini na kuipokea Injili ya Kristo. Kweli _____ Hapana _____

**MSTARI WA KUKARIRI KWA SOMO HILI: WAEFESO 2:8,9**

*"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu; ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu."*

Watu wengi wanafikiri Mungu anahitaji watu kuwa wenye haki, wanaoishi vema, wakiwa na maisha adilifu, kabla hawajaokolewa. Yesu alisema, *"Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi"* (Mathayo 9:13b). Alisema hivyo wakati alikuwepo hapa duniani. Baadaye, kutoka mbinguni, ambapo amekaa katika mkono wa kulia wa Mungu Baba, alituma ujumbe wake kwa ajili ya Kanisa lililo Mwili wa Kristo kumpitia Paulo, mtume kwa Mataifa. Katika ujumbe huu Yesu aliongea kuhusu kuhesabiwa haki.

19. (Warumi 5:1) Tumepataje kuhesabiwa haki? _____

    Tunapata nini wakati tunapohesabiwa haki? _____

20. (Wagalatia 2:16) Haiwezekani kuhesabiwa haki kupitia njia gani? _____

21. Soma Warumi 3:28. Hitimisho gani linaweza kutolewa kwa mstari huu? _____

    _____

**VIFAA VIKALI AU BUTU?**

na Irving D. Larson

*"Maana Neno la Mungu li hai na lina nguvu na kali kuliko upanga uwao wote…"* (Waebrenia 4:12)

Tatizo moja ambalo waseremala wanakutana nalo ni kutumia vifaa ambavyo siyo vikali kama inavyotakiwa. Mseremala yeyote aliye mzuri anajua kuwa kifaa kikali ni hatua ya kwanza katika kufanya kazi nzuri. Kifaa kikali hufanya kazi kuwa rahisi zaidi, na matokeo ni kazi inayopendeza zaidi. Ninapenda hadithi moja kuhusu mkata kuni wa zamani aliyepewa msumeno wa mashine kwa mara ya kwanza. Alikata magogo mawili ya kuni alipotumia mashine hiyo katika siku ya kwanza. Lakini katika siku iliyofuata alikata kuni nyingi zaidi baada ya mtu mmoja kumwonesha jinsi ya kuwasha mashine hiyo (maana yake siku ya kwanza alitumia mashine bila kuiwasha – ni utani tu). Yeyote aliyezoea kukata kuni na msumeno au shoka anafahamu kwamba nguvu nyingi zaidi inahitajika ikiwa vifaa hivyo ni butu na kazi ni rahisi ikiwa viko vikali. Katika Mhubiri 10:10 tunasoma, *"Iwapo chuma hakipati, wala mtu hakinoi; Ndipo hana budi kutumia nguvu zaidi. Walakini yafaa kutumia hekima, na kufanikiwa."*

Sisi waumini tunaweza kujifunza kutokana na mfano huu. Tumepata kifaa kikali kutumia katika maisha yetu, yaani Neno la Mungu. Neno la Mungu ni lenye *"ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili."* Ni mara ngapi tunajaribu

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

kuwashawishi na kuwabadilisha watu kwa kutumia hoja za akili zetu tu, badala ya kulitumia Neno la Mungu na kuyaruhusu Maandiko kupenye ndani ya mioyo ya watu! Barua ya Paulo kwa Timotheo inaongea kuhusu *"Mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."* Tujitahidi kuwa watenda kazi wanaofanana na huyu katika 2 Timotheo 2:15.

Tumejifunza yafuatayo hadi hapa katika somo hili:

1. Ukweli wa Mungu unafunuliwa katika Neno lake.
2. Biblia inafundisha kwamba mtu wa asili anaweza kubadilika kuwa mtu wa kiroho.
3. Kubadilika kutoka mtu wa asili kuwa mtu wa kiroho ni kuwa "kiumbe kipya."
4. Njia ya kuhesabiwa haki ni kwa imani katika Yesu Kristo.
5. Mungu alifunua habari za kuhesabiwa haki kwa imani kupitia Mtume Paulo.

Baada ya kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi, sisi ni "watoto" katika Kristo tukihitaji kuendelea kukua katika maisha yetu mapya. Mungu ametupatia Biblia itusaidie kukomaa kiroho. Katika kujifunza Biblia mwanafunzi mwenye hekima atakumbuka kuomba akimwambia Baba ayafungue macho yake ya ufahamu.

# SEHEMU YA TATU

## MATOKEO YA DHAMBI

1. Rejea Warumi 5:12

   a. Dhambi iliingiaje ulimwenguni? _____

   b. Matokeo ya kuingia kwa dhambi ulimwenguni ni nini? _____

   *"Kwa kuwa wote wamefanya dhambi na kupungukiwa wa utukufu wa Mungu"* (Warumi 3:23)

2. Rejea Warumi 6:23

   a. Malipo ya dhambi ni nini? _____

   b. Zawadi (karama) ya Mungu ni nini? _____

   c. Tunaipokea zawadi hii kumpitia nani? _____

**SOMO MAALUMU:** Kabla hujaendela soma sura nzima ya kwanza ya kitabu cha Warumi. Fikiria hukumu ya Mungu juu ya watu wenye dhambi, na hukumu ya wale *"waipingao kweli kwa uovu"* (Warumi 1:18)

3. Rejea Warumi 1:21-25. Katika maneno yako mwenyewe eleza nini kinatokea kwa mtu ambaye lengo lake siyo juu ya Mungu. _____

   _____

4. (Warumi 6:21) Nini tunda (tokeo) la maisha la ubinafsi na dhambi? _____

5. (Wagalatia 5:19-21) Matendo ya mwili yalivyoorodheshwa katika Maandiko ni matendo gani? _____

   _____

   _____

6. (Wagalatia 5:22-23) Matunda ya Roho ni matunda gani? _____

   _____

7. Mtu akikuuliza namna ya kuwa Mkristo, yaani, jinsi ya kupata uzima wa milele, ungemshirikisha mstari au mistari gani ya Neno la Mungu? Zungusha uchaguzi wako:

   1 Wakorintho 15:3-4 Warumi 5:8 Mathayo 7:12 Warumi 10:9

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

ZINGATIA: "Kuhuishwa" katika Neno la Mungu ni "kufanywa hai". Neno la Mungu hueleza kitendo cha "kufanywa hai" kwa maneno mbalimbali. Kwa mfano: "Kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3), "Kumpokea yeye" (Yohana 1:12), na "Kuamini" (Warumi 10:9 na Yohana 3:16).

8. (1 Wathesolanike 2:12) Baada ya mtu "kuhuishwa," au "kufanywa hai," Mungu hutegemea nini kutoka mtu huyu? _____

9. (1 Wathesolanike 2:13) Kwa waumini wa Thesolanike, "mwenendo mzuri" ulianza wakati "walipopokea Neno la Mungu." Neno la Mungu hufanya nini kwa wale wanaoamini? _____

10. 2 Timotheo 2:15 ina mafundisho gani kwetu? _____

    _____

    _____

    Tutakuwa "tunatembea kwa kumpendeza Mungu" kama tunayatii mafundisho haya? Ndiyo____ Hapana_____

ZINGATIA: *"Kulitumia kwa halali"* Neno la Mungu unatakiwa kutambua kuwa Mungu hajashughulika na watu kwa njia moja katika kipindi chote cha kihistoria. Kuna mabadiliko mengine yaliyofanyika ndani ya historia wakati Mungu alipoendelea kufunua mpango wake kwa wanadamu. Waisraeli walikuwa na manabii katika Agano la Kale, Wayahudi walikuwa na mitume kumi na wawili katika Agano Jipya, na Mataifa walikuwa na mfano mwingine wa kufuata.

11. Bwana Yesu Kristo amechagua "kielelezo" au "mfano" kwa ajili yetu kufuata.
    a. (1 Timotheo 1:1) Nani anaongea? _____
    b. (1 Timothy 1:16) Kristo alikusudia nani kuwa "kielelezo" au "mfano"? _____
    c. (1 Timotheo 1:15) Paulo anajieleza kivipi? _____

12. a. (Waefeso 3:1) Paulo anasema yeye ni nani? _____
    b. (Warumi 15:16) Nani alifanywa kuwa mtumishi kwa Mataifa? _____
    c. (Warumi 15:15,16) Nani alimfanya Paulo kuwa mtumishi? _____

13. Kuna mafundisho gani kwa waumini katika 1 Wakorintho 11:1?_____

    _____

14. Tumfuate Paulo katika njia zipi? Elezea Wafilipi 4:9 katika maneno yako mwenyewe. _____

    _____

15. Kwa nini "kielelezo," au "mfano," awe Paulo na siyo mitume wengine? Soma mistari yote hii kabla hujajibu: Wagalatia 2:7; Waefeso 3:1-3, 7-9 na Wakolosai 1:25. _____

    _____

ZINGATIA: Katika nyakati zilizopita Mungu aliwachagua watu fulani kuwa viongozi wa watu wake wateule, Israeli. Mmoja wa viongozi hawa wakubwa alikuwa Musa, aliyewatoa Waisraeli kutoka Misri kwa kuvuka Bahari Nyekundu. Agano la Kale linaeleza jinsi watu walivyomwasi mteule huyu wa Mungu mara kwa mara. Walishindwa kumtii Mungu, walipokataa kumfuata kiongozi wake mteule. Tambua kwamba Musa alichaguliwa na Mungu kuwa Mtoa Sheria kwa Israeli. Paulo alichaguliwa kufunua ujumbe mpya maalamu ambao unaitwa "ufunuo wa siri." Linganisha Kutoka 20:1-17 na Warumi 16:25.

16. (Waefeso 3:8,9) Lengo takatifu la Mungu katika kuwa na mjumbe maalumu kwa ajili ya Mataifa ni nini?

    _____

    _____

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*

17. "Siri ya Kristo" ni nini katika Waefeso 3:6? _____

_____

18. Linganisha Waefeso 3:8,9 na Mathayo 10:5,6. Kristo, katika huduma yake duniani, aliwaamuru mitume kumi na wawili wasiwaende watau gani? _____

Hata katika sura za kwanza za kitabu cha Matendo, Petro na mitume wengine waliwahubiria Wayahudi tu jinsi walivyoagizwa na Yesu (Matendo 2:14, 22; 3:12). Lakini Paulo aliwaandikia wanadamu wote kuhusu ujumbe aliopewa na Kristo kama alivyoagizwa. Jambo hili linaonesha badiliko katika mahusiano kati ya Mungu na wanadamu mbalimbali kupitia historia.

19. Mungu alikuwa na mipango tofauti kwa ajili ya taifa la Israeli na kwa ajili ya Kanisa la leo. Agizo lake kwa ajili ya Kanisa lililo Mwili wa Kristo limeelezwa wazi katika 2 Wakorintho 5:18-20. Mistari hii inasema nini? _____

_____

_____

UJUMBE WA MUNGU KWA LEO: "*Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani* (Mataifa)*; maana yeye yule ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao*" (Warumi 10:12).

Kumbuka kwamba hatuwezi kujifunza mapenzi ya Mungu na mipango yake kwa ajili yetu katika Biblia tukisoma Biblia kwa njia ya kupita juu juu kama mtu anayesoma kwa ajili ya starehe. Tunatakiwa kuonesha tumekubaliwa na Mungu, watenda kazi wasio na sababu ya kutahayari, tukitumia kwa halali neno la kweli. Kufaulu katika wajibu huu tutahitaji kusoma Biblia kila siku na kuchunguza kwa ndani ili tuelewe ujumbe wa Mungu kwa ajili yetu.

**Tumia nafasi hii kuandika maswali au maoni yoyote uliyo nayo:**

_____

_____

_____

_____

_____

_____

**Rudisha somo hili kwa:**

_____ Namba yetu ya simu_____

_____

_____

**Habari zako:**

Tarehe: _____ Jina lako:_____

Anwani yako: _____

Mji: _____Namba yako ya Simu:_____

*Copyright © 2018 Prison Mission Association – Kanisa la Neema – Bible Correspondence Fellowship*